# UQAB

Jarida la



*Toleo 26 - Jamad-al-thani 1440 H / Machi 2019 Miladi*

**Je, Wakati Haujawadia wa Kuipa China Funzo Lisilo Sahaulika?**


**Kwa Nini Xinjiang ni Muhimu kwa Uchina**

**Kimya Kizito kutoka Kwa Tawala za Waislamu**

**Mateso ya Waislamu wa Uyghur**

**Kizazi cha Watoto wa Uyghur Kinaibwa na Uchina**

**Tunaungana naa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**




**#الخلافة_تحرر_تركستان_الشرقية**

**#Khilafah_Liberates_EastTurkestan**

بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَٰنِ الرَّحِيمِ

**Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

﴿وَعَدَ اللَّهُ الَّذِينَ آمَنُوا مِنكُمْ وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ لَيَسْتَخْلِفَنَّهُمْ فِي الْأَرْضِ كَمَا اسْتَخْلَفَ الَّذِينَ مِن قَبْلِهِمْ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمْ دِينَهُمُ الَّذِي ارْتَضَىٰ لَهُمْ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّن بَعْدِ خَوْفِهِمْ أَمْنًا ۚ يَعْبُدُونَنِي لَا يُشْرِكُونَ بِي شَيْئًا ۚ وَمَن كَفَرَ بَعْدَ ذَٰلِكَ فَأُولَٰئِكَ هُمُ الْفَاسِقُونَ﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

# Kampeni ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir Vita vya Uchina Dhidi ya Uislamu ndani ya Turkestan Mashariki Vitasitishwa na Khilafah Rashidah

Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir imezindua kampeni pana ya kufichua ukweli kutokana na mzozo wa Uchina na Waislamu walioko Turkestan Mashariki ambao wanaendelea kupitia kampeni ya mauaji kutoka kwa Uchina tangu 1863. Zaidi ya Waislamu wa Uyghur milioni moja wamefariki ndani ya mashambulizi yaliyotokea mnamo 1949 ambapo utawala wa Kikomunisti wa Uchina ukiongozwa na Mao Zedong ulipochukua hatamu na kupiga marufuku uhuru wa eneo hilo na kuliteka kuwa ni sehemu ya Uchina. Waislamu wa eneo hilo walihamishwa na kutawanywa ndani ya mikoa ya Uchina. Lakini Waislamu wa Uyghur waliokuwa na misimamo hawakujisalimisha kwa Wachina; wakaleta mwamko wa mapinduzi mnamo 1933 na 1944 na mapinduzi yakaendelea ndani ya eneo hilo dhidi ya uvamizi wa Uchina kama ilivyokuwa mnamo 2009.

Uislamu ndio sababu msingi ya chuki ya kudumu kutoka kwa Wachina dhidi ya Waislamu wa Uyghur. Misikiti yao ni miongoni inayolengwa na Uchina katika muendelezo wa sumu yake dhidi ya Uislamu. Ilivunja takribani misikiti elfu 25 mnamo 1949 na takribani misikiti 500 pekee ndio iliyobakishwa ndani ya eneo hilo kubwa. Leo, Uchina imeachana na nusu ya ukomonisti wake katika “uchumi” lakini bado inaendelea kupambana na athari zozote za udini hususan miongoni mwa vijana. Hii ndio sera ya kikweli inayofanyiwa kazi na Uchina ndani ya eneo hilo.

Licha ya yote hayo. nishati ya Waislamu inaendelea  kuwepo ndani ya Turkestan Mashariki ambayo imewezesha kurudi tena kwa athari za Uislamu katika maisha, hususan vijijini. Mtafaruku uliolikumba eneo hilo unaendelea kila wakati mpaka sasa na umelifanya kuwa eneo tofauti na mengine kutokana na ukosefu wa utulivu kwa sababu ya mabomu na vitendo vya vurugu dhidi ya serikali na maamuzi ya kutaka kujitenga. Hatima yake ni imekuwa sehemu dhaifu ndani ya serikali. Kwa kujibu hilo, Uchina inafuatilia kwa makini maisha ya Waislamu wa Uyghur na kuvidhibiti vyombo vya habari kutofuatilia mauaji na kamatakamata inayofanya katika kiza kwa kutumia nguvu ndani ya eneo hilo. Pia inawafuatilia Waislamu wa Uyghur waliotoroka na walio na sauti nje chini ya kisingizio cha “ugaidi” imefaulu kuwashika wengi kupitia njia za kiusalama wa kimataifa hususan kutoka nchi za Asia ya Kati na Pakistan.

Lakutia msumari wa moto ni kuwa dhuluma hizi za Uchina dhidi ya Waislamu wa Uyghur zinafanyika mbele ya macho na masikio ya mamilioni ya Waislamu duniani pasi na wao kushinikiza dhuluma hizi kuondoshwa. Hii ni kwa sababu mamilioni ya Waislamu wametapakaa na hawakuunganishwa pamoja chini ya dola, dola ya Ummah, dola ya Uislamu kukosekana kwa Khilafah ambayo kila Muislamu aliye na uwezo lazima afanye kazi kuirudisha tena na kumtafuta Khalifah, imamu anayesimamia mambo kwa uzuri na mwenye kulinda na kuwa ngao ambayo nyuma yake Waislamu wanapigana, kama ilivyosimuliwa katika Sahih Al-Bukhari kutoka Abu Huraira (ra) aliyesema: Mtume (saw) alisema: «وَإِنَّمَا الإِمَامُ جُنَّةٌ يُقَاتَلُ مِنْ وَرَائِهِ وَيُتَّقَى بِهِ» **“Hakika Imamu ni ngao kutoka nyuma yake munapigana na munajilinda.”** Na kisha Uchina na wengine hawatojaribu kuwadhuru Waislamu kwa sababu watafahamu kuwa ukandamizaji wao utafuatiwa na malipo maradufu. Hakika Mwenyezi Mungu ana nguvu na muweza.

**Ijumaa, Jumada I 1440 AH -25 Januari 2019 M**



**Email: info@uqab.or.ke**

Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir

بسم الله الرحمن الرحيم

﴿وَعَدَ ٱللَّهُ ٱلَّذِينَ ءَامَنُواْ مِنكُمۡ وَعَمِلُواْ ٱلصَّٰلِحَٰتِ لَيَسۡتَخۡلِفَنَّهُمۡ فِي ٱلۡأَرۡضِ كَمَا ٱسۡتَخۡلَفَ ٱلَّذِينَ مِن قَبۡلِهِمۡ وَلَيُمَكِّنَنَّ لَهُمۡ دِينَهُمُ ٱلَّذِي ٱرۡتَضَىٰ لَهُمۡ وَلَيُبَدِّلَنَّهُم مِّنۢ بَعۡدِ خَوۡفِهِمۡ أَمۡنٗاۚ يَعۡبُدُونَنِي لَا يُشۡرِكُونَ بِي شَيۡـٔٗاۚ وَمَن كَفَرَ بَعۡدَ ذَٰلِكَ فَأُوْلَٰٓئِكَ هُمُ ٱلۡفَٰسِقُونَ﴾

REF: 012/1440 | Ijumaa, 19 Jumada I 1440 AH | 25/01/2019 CE

# Je, Wakati Haujawadia kwa Mateso ya Waislamu wa Uyghur Kumalizika?
# Je, Wakati Haujawadia wa Kuipa China Funzo Lisilo Sahaulika?

**Taarifa kwa vyombo vya habari**

Katika miezi ya hivi karibuni tulisikia ripoti za habari za kupamba moto kwa ukatili wa sera kali za China kwa Waislamu wa Uyghur wanaoishi Mashariki mwa Turkistan, nchi nzuri iliyo Mashariki mwa ardhi ya Waislamu. Haikutulia tangu kunyakuliwa na Mao Zedong utawala wa Kikomunisti wa China mnamo 1949 aliyeliunganisha na eneo la China baada ya kuwauwa zaidi ya Waislamu wa Uyghur milioni moja na kuvunja misikiti elfu 25. Habari za hivi punde lakini zisizo za mwisho za uchunguzi ulioripotiwa na Jarida la Atlantiki na vyombo vyenginevyo vya habari kama BBC na Al-Jazeera, kwamba China inazuilia karibu Waislamu milioni moja katika mkoa wa Turkistan Mashariki katika kambi zake za uzuizi! Uchunguzi huo uliwanukuu wajuzi kutoka Umoja wa Mataifa, kuwa lengo la kambi hizo ni uchafuzi wa kifikra kwa Waislamu wa Uyghur eneo hilo, ili waachane na Uislamu, na inajulikana vyema kuwa China ni mojawapo ya nchi zilizo dhidi ya Uislamu wazi wazi, jarida hilo la kijasusi limechapisha tangazo la China kuwa Uislamu ni maradhi yanayo ambukiza na ni lazima yatibiwe kwa kila njia, hata kupitia mateso na mauwaji.

Uhalifu ndani ya Turkistan Mashariki hauelezeki. Ndugu zetu huko wanafungwa na kunyongwa katika vigogo vya miti, simiti na zege zinamwaga midomoni mwao kuwaziba pumzi, dada zetu wanazuiwa kushika mimba na kuzaa, wanaume wanahasiwa. Serikali ya kikafiri ya China inaweka Mchina kafiri katika kila nyumba ya Muislamu ili kuwachunguza chini ya kisingizio cha kuwaelimisha utamaduni wa Kichina, wakipuuzilia mbali faragha yao na matukufu yao. Waislamu wanazuiwa kufunga mwezi Mtukufu wa Ramadhan. Waislamu wanalazimishwa kuukana Uislamu chini ya tishio la mateso ya kisaikolojia na kimwili, kwa mujibu wa Shirika la Haki za Kibinadamu. Mamlaka za China zinadai kuwa zinalazimishwa kukabiliana na kilele cha uhalifu: ugaidi na mfumo wenye misimamo mikali na kulingania kujitenga, kama ilivyo ripotiwa na shirika la habari la BBC. Chini ya miito hii ya kirongo mamlaka hizo zinatekeleza vitendo kadha wa kadha vya kinyama.

Haya yanawatokea Waislamu wa Uyghur eneo la Turkistan Mashariki, na hakuna anayenyosha kidole, hakuna hata shutuma na kukemea madhalimu na watawala wahalifu wa Waislamu wameweza kufanya, kana kwamba Waislamu wa Uyghur sio katika Umma wa Kiislamu, kana kwamba ushindi wao sio wajib juu yao na juu ya Ummah wa Kiislamu! Je, kwani hawajasikia maneno ya Allah, Mtakatifu na Aliye tukuka:

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَالْوِلْدَانِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَا أَخْرِجْنَا مِنْ هَٰذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ أَهْلُهَا وَاجْعَلْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ وَلِيًّا وَاجْعَلْ لَنَا مِنْ لَدُنْكَ نَصِيرًا

"Na muna nini nyinyi (mpaka) hamupigani katika njia ya Allah na (kwa ajili ya) wanyonge wanaume, wanawake na watoto ambao wanasema, 'Mola wetu tutoe katika kijiji hichi cha watu madhalimu na utujaaliye kutoka kwako mtetezi na utujaaliye kutoka kwako mwenye kutunusuru" [An-Nisa: 75]

Turkistan Mashariki ilikuwa ni sehemu muhimu ya dola ya Kiislamu. China haikusubutu kuiunganisha hadi baada ya Khilafah Uthmaniyya kuvunjwa na ardhi za Waislamu kugawanywa kuwa idadi ya vidola 50.

*Endelea Uk..4*

**Enyi Waislamu:**

Ni nini kinachoifanya China kusubutu kuikalia Turkistan?

Ni nini kinachoifanya China kusubutu kuwagandamiza na kuwanyanyasa Waislamu wa Uyghur?

Je, si kwa sababu ya kuwa wamepoteza mchunga anaye chunga mambo yao, wamempoteza Imam muadilifu ambaye hupigana nyuma yake na kuhifadhiwa naye, wamempoteza Khalifah Muongofu anayejibu vilio, kelele na manung'uniko yao?

**Enyi Waislamu:**

Simameni na muwasaidie ndugu na dada zenu, Waislamu wa Uyghur na Waislamu wote walio kandamizwa Mashariki na Magharibi mwa dunia; kupitia kufanya bidii pamoja na Hizb ut Tahrir ili kuasisi dola ya Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume, itakayozikomboa ardhi zilizo nyakuliwa za Waislamu, na kuziacha huru shingo za Waislamu kutokana na uimla na ukoloni katika aina zake zote, na itawaadhibu wale walio wakandamiza na itampiga kwa mkono wa chuma yeyote atakayewaza tu kushambulia matukufu ya Uislamu na Waislamu.

**Enyi Waislamu:**

Sisi katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir tunatangaza kuzindua kampeni kubwa kwa anwani "Vita vya China Dhidi ya Uislamu eneo la Turkistan Mashariki Vitamalizwa Pekee Kupitia Khilafah Rashidah" ili kuwasaidia ndugu zako na dada zako wa Kiislamu eneo la Turkistan Mashariki, hivyo basi shiriki na sambaza maalumati zake mbali iwezekanavyo. Huenda ulinganizi wetu ukafika masikioni mwa vijana miongoni mwa watu wenye nguvu na ulinzi, na huenda wakawajibu walinganizi wa Allah na kuisaidia Dini Yake ili kusimamisha dola ya kweli (Haq), Dola ya Mtume wa Allah (saw), dola ya Khilafah Rashida ya pili kwa njia ya Utume.

**وَيَوْمَئِذٍ يَفْرَحُ الْمُؤْمِنُونَ * بِنَصْرِ اللَّهِ يَنصُرُ مَن يَشَاء وَهُوَ الْعَزِيزُ الرَّحِيمُ * وَعْدَ اللَّهِ لا يُخْلِفُ اللَّهُ وَعْدَهُ وَلَكِنَّ أَكْثَرَ النَّاسِ لا يَعْلَمُونَ**

"Na siku hiyo waumini watafurahi* Kwa Nusra ya Allah. Humnusuru amtakaye na Yeye ndiye mwenye nguvu Mwenye kurehemu* (Hii ni) ahadi ya Allah, Allah havunji ahadi yake lakini wengi wa watu hawajui" [Ar-Rum: 4-5]

**Linki ya kampeni:**

http://www.hizb-ut-tahrir.info/en/index.php/hizbuttahrir/16793.html

**Hashtag ya Kampeni:**

#الخلافة_تحرر_تركستان_الشرقية

#Khilafah_Liberates_EastTurkestan

**Dkt. Osman Bakhach**
**Mkurugenzi wa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Kwa Nini Xinjiang ni Muhimu kwa Uchina

Ukandamizaji wa Uchina wa kupita mipaka dhidi ya Waislamu haujawahi kushuhudiwa duniani kote. Mwaka uliopita umeshuhudia matukio ya ripoti na video zikionesha Waislamu wa Uyghur wakijazwa ndani ya kambi zilizotapakaa ndani ya magharibi ya Uchina. Huku shinikizo zikizidi kutoka katika vyombo vya habari vya Magharibi, ambavyo vina ajenda yao, sasa utawala wa Uchina umekubali kuwa inatekeleza unyama huo: kisiwa cha kambi kimejengwa. Shirika la habari linaloendeshwa na serikali ya Uchina la Xinhua siku ya Jumamosi 13 Oktoba 2018 lilimnukuu afisaa rasmi kuwa lazima dini zipitie "mchakato wa kuzifanya mujtamaa zisizokuwa za Kichina kuwa chini ya athari ya thaqafa ya Kichina." Licha ya Uchina kuinuka kiuchumi kimiujiza, inaendelea kutapatapa dhidi ya eneo hili ambalo halijamakinika, lakini ni muhimu kwa Uchina na sio tu kimikakati bali hata kwa maisha yake.

Eneo Huru la Xinjiang la Uyghur (XUAR) lipo upande wa kaskazini magharibi ya Uchina na limetapakaa kwa kilomita mraba milioni 1.6. Eneo hili linajumuisha moja kwa sita ya eneo la Uchina na linapakana na nchi nane. Leo Xinjiang ni nyumbani kwa watu milioni 21 wanaotoka katika makabila kumi na tatu na kubwa likiwa ni la Waislamu wa Uyghur. Kihistoria eneo hili limekuwa kitovu msingi cha kiuchumi na kubadilishana thaqafa kati ya Mashariki na Magharibi, Xinjiang ilikuwa kitovu muhimu cha Barabara ya Siliki. Kuzidi kwa ukandamizaji wa Ulaya miaka ya 1800 kulipelekea kupanuka kwa Falme za Urusi na Uingereza ndani ya Asia ya Kati. Ufalme wa Urusi ulizidisha athari yake katika mipaka ya kaskazini mwa Uchina katika Karne ya 19 na kwa sababu hiyo Ufalme wa Qing ukalitia eneo hilo chini ya udhibiti wake na kubuni Xinjiang kama mkoa rasmi wa Uchina mnamo 1884. Lakini utawala huo ulipata mashambulizi ya mara kwa mara kutoka kwa Waislamu wa eneo hilo na katika nusu ya Karne ya 19 ambapo Uchina chini ya Qing ilipoingia katika Vita vya Madawa ya Kulevya, muendelezo wa mashambulizi ya ndani na kuingiliwa na mkono wa nje; kwa hivyo haikuweza kuwekeza jeshi lenye nguvu ndani ya Xinjiang. Kuanguka kwa Ufalme wa Qing mwaka 1911 ukapelekea udhibiti wa Uchina katika eneo la Xinjiang kuondoka kabisa. Ikamchukua Mao Zedong hadi mwaka 1949 kupiga marufuku uhuru wa eneo hilo na kuliteka kuwa chini ya Jamhuri ya Zedong. Mara hii Mao alijaribu kuwatawanya katika mikoa mengine wakaazi wa eneo hili Waislamu kwa kutumia nguvu na kuwahamisha Wachina wa Han kwenda katika eneo hilo. Sera hii bado inaendelea hadi leo lakini imefeli kwa ukamilifu wake na kilele chake ni uasi wa Ürümqi mnamo 2009.

Xinjiang inawakilisha eneo moja kati ya maeneo manne kama ngao ya Uchina. Maeneo ngao yanaulinda moyo wa ardhi ya Uchina. Moyo wa ardhi ya Uchina umegawanyika vipande viwili, kaskazini na kusini ambayo zinawakilishwa na lugha mbili msingi, Kimandarini kutoka kaskazini na Kikantoni kutoka kusini. Moyo wa ardhi ya Uchina ipo katika mito miwili mikubwa –Mto wa Yelo kaskazini na Yangtze kusini. Moyo wa ardhi ya Uchina ni eneo la kilimo.  Idadi ya waHan haikusambaa kote ndani ya moyo wa ardhi ya Uchina. Idadi kubwa ya watu iko mashariki kwa sababu magharibi ya Uchina haina mvua nyingi na hivyo haiwezi kuhimili idadi kubwa ya watu. Hivyo basi Uchina ni nchi nyembamba mno, ikiwa na idadi kubwa ya watu waliotapakaa. Mjumuiko wa maeneo yasiyokuwa ya waHan yanauzunguka moyo wa ardhi –Tibet, Mkoa wa Xinjiang, Mongolia ya Ndani na Manchuria. Haya ndio maeneo ngome ambayo kihistoria yamekuwa chini ya utawala wa Uchina wakati Uchina ilipokuwa na nguvu na yakajitenga wakati Uchina ilipokuwa dhaifu au yametumiwa na dola za nje zenye nguvu ili kuingilia kati ndani ya Uchina. Haya pia ndio maeneo kihistoria ambayo ni chimbuko la vitisho dhidi ya Uchina. Lakini kando na kuwa ni maeno ngome, kuyadhibiti yanaipa Uchina nguvu ya kujilinda. Hivyo basi Xinjiang ni moja ya maeneo manne ambayo ni muhimu kwa umakinifu wa himaya ya Uchina.

Maajabu ya uchumi wa Uchina yamehusishwa na kuwepo kwa kawi na bidhaa. Xinjiang ni eneo muhimu ambalo linalohitajika kuendesha uchumi wa Uchina na pia lipo mahali muhimu kimikakati kama njia ya usambazaji. Xinjiang ina asilimia 20 ya makaa, gesi ya kawaida, na hazina za mafuta. Xinjiang ina idadi kubwa ya hazina ya kawi kuliko maeneo yote nchini humo, Mafuta yaliyoko katika Karamay ni mengi ndani ya Uchina yote na eneo hilo lina makaa mengi, fedha, shaba, chuma, naitreti, dhahabu na zinki. Xinjiang ni eneo kubwa ndani ya Uchina linalotoa gesi ya kawaida na ndio kitovu cha biashara na njia za mabomba ya mafuta kutoka eneo la Asia ya Kati na kwengineko. Xinjiang pia ni sehemu ya Uchina ya kuwekeza zaidi rasilimali zake za mafuta kwa kuwa eneo hilo pia ni njia muhimu ya usafirishaji. Xinjiang ni eneo pekee ndani ya Uchina ambalo linapakana na jamhuri za Asia ya Kati, mafuta ya Asia ya Kati (na idadi kubwa ya mafuta ya Urusi) yanaingilia kwa kupitia mabomba ya Uchina yaliyoko Xinjiang. Bomba la kwanza la mafuta la kimataifa lililowahi kujengwa ni Bomba la Mafuta la Kampuni ya Sino-Kazakh ambalo lilianza kupiga mafuta kuanzia Julai 2006. Bomba hili lilianza kutoka Atasu kaskazini Kazakhstan likaingia eneo la Xinjiang katika mpaka wa Kazakh-Uchina katika Alashankou na kuishilia katika PetroChina Dushanzi. Ilhali Xinjiang haikujumuishwa katika miujiza ya Uchina lakini kiukamilifu hiyo ndio inayoimakinisha Uchina na kwa sababu hiyo ni eneo muhimu la kimikakati.

*Endelea Uk..6*

Kuinuka kwa Uchina ilipelekea kuundwa kwa Maeno Maalumu ya Kiuchumi (SEZ) katika meaneo ya pwani ya Uchina ambapo bidhaa zinatengenezwa kwa usafirishaji duniani kupitia bahari. Tatizo la Uchina ni kuwa limeufanya uchumi wake kutegemea njia za bahari lakini Uchina haina uwezo wa kijeshi wa kuweza kutoa ulinzi kwa njia zake za usambazaji baharini. Kwa sababu Jeshi la Bahari la Amerika linadhibiti bahari duniani na kufungiwa njia visiwa vinavyoizunguka Uchina katika eneo linatepelekea kusambaratika kwa uchumi wake. Hii ndio inaipelekea Xinjiang kuingia katika hesabu kwani kihistoria Uchina imekuwa ikiitumia kama njia ya ardhini kuelekea duniani. Magharibi ya Uchina inapeana nafasi kubwa njia za Bahari ya Arabia kupitia Pakistan hadi kwa Bahari ya India na Guba ya Fursi. Uchina inaweza kupitia Pakistan, Asia ya Kati, Mashariki ya Kati na eneo lote la Eurasia (mjumuiko wa Ulaya na Asia) na zaidi kupitia Xinjiang na kusafirisha rasilimali zake kwa njia ya ardhini na kuepuka kutegemea kupindukia kwa njia za bahari zisizotegemeeka. Ni kwa sababu hii ndio Uchina kupitia mkakati wake mkubwa wa Mpango wa Ukanda na Barabara (BRI) utakuwa na vitengo kadhaa vikipitia Xinjiang ili kuunganisha nchi yote na Eurasia na zaidi. Kwa kutumia njia hiyo, Xinjiang imekuwa kijiografia muhimu mno kufikia uunganishaji wa kiuchumi kwa Eurasia yote. Mpango mzima wa BRI unaahidi kuwa na athari kubwa juu ya mahusiano ya kibiashara ya Uchina na athari yake kimataifa na katikati ya hilo ni Xinjiang.

Sababu za kimikakati, kiuchumi, kibiashara, kiidadi ya watu na kisiasa zinaifanya Xinjiang kuwa ni suala la kimaisha (kufa kupona) kwa Uchina. Lakini licha ya kutumia pesa nyingi katika eneo hilo na hapo awali kutumia mkono wa chuma imefeli kuwavutia Waislamu katika eneo hilo. Ilhali vyombo vya habari vya kimagharibi hivi sasa ndio vimeangazia yanayofanywa na Uchina. Mikakati ya Beijing inafuata nyayo za Magharibi ambao wanamipango sawa na hiyo yakuwa shughulikia Waislamu, ambao kwa muda mrefu wameng'ang'ana kuwaunganisha. Njama hizi zimefeli huko Magharibi na haina shaka zitafeli ndani ya Uchina. Suala linalo waumisha vichwa viongozi wa Uchina ni kuwa uchumi na siasa zao za usoni zinapitia katika eneo ambalo lina idadi kubwa ya Waislamu ambao Beijing imekuwa ikiwapiga vita kwa zaidi ya karne.

**Imeandikwa Kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahri na**

**Adnan Khan**

# Habari & Maoni
# Kimya Kizito kutoka Kwa Tawala za Waislamu huku Uchina Ikiendeleza Kampeni yake ya Kidhalimu ya Kishirikina Dhidi ya Waislamu

**Habari**:

Siku ya Jumamosi, 5 Januari, gazeti pekee la Uchina la Kiengereza, Global Times liliripoti kuwa serikali ya Uchina ilipitisha sheria ya kuufanya Uislamu uwiane na ujamaa. Gazeti hilo likasema kuwa maafisa wa serikali, "walikubali kuungoza Uislamu uendane na ujamaa na kutekeleza mikakati ya kuzifanya dini zipitie mchakato wa kuzifanya mujtamaa zisizokuwa za Kichina kuwa chini ya athari ya thaqafa ya Kichina" ndani ya miaka 5 ijayo. Mwanzoni mwa mwezi huu, watawala nchini Uchina katika mkoa wa Yunnan walifunga misikiti 3 iliyobuniwa na Waislamu wanaokandamizwa kutoka kabila dogo la waHui

**Maoni**:

Matukio haya mapya kutoka kwa utawala wa Uchina ni muendelezo wa kampeni yake ya kidhalimu ili kuuondosha Uislamu kutoka kwa watu Waislamu na kuwalazimisha kufuata imani ya kishirikina kupitia vitisho na uoga. Utawala huo tayari umepiga marufuku katika baadhi ya maeno yake –kufunga saum, kuvaa mavazi ya Kiislamu, kufuga ndevu, na watoto wa chini ya miaka 18 kutoingia msikitini kusikiliza Khutbah. Serikali pia imeharamisha wazazi kutowapa watoto wao wanaowazaa majina fulani ya Kiislamu na kutowapa watoto wao elimu ya Kiislamu au kutoshiriki katika amali za Kiislamu. Hii ni pamoja na kuwashinikiza Waislamu wa Uyghur waoe watu wasiokuwa Waislamu kutoka katika waHan.  Mwaka 2016, katika mpangilio wake wa kupambana na Uislamu utawala huo ulizindua "Kampeni ya Kuwa Familia" –nidhamu ambayo maafisaa waHan kuhamia kwa muda na kuishi na familia za Waislamu ndani ya Xinjiang ili kuchunguza na kuripoti juu ya ishara zozote za wenyeji wao za kujifunga na Uislamu au 'misimamo mikali' –ikijumuisha kukataa pombe, kuswali Jum'a, kufunga Ramadhan, au hata kuweka picha ukutani zikiwa na maandishi ya Kiislamu. Mnamo Disemba 2017, watawala ndani ya Xinjiang waliita jeshi zaidi ya milioni moja kuja kukaa kwa wiki moja na Waislamu wa Uyghur nyumbani mwao kwa lengo hilo. Amal nyingine msingi za Kiislamu zimebandikizwa kuwa misimamo mikali mfano kama kuchagua kula chakula Halali na kutoa salamu za Kiislamu. Viongozi wa Chama cha Kikomunisti ndani ya Urumqi mji mkuu wa mkoa wa Xinjiang walizindua kampeni dhidi ya bidhaa Halali, vitengo vinavyoiongoza vikiapa "kupigana vita vya mwisho" dhidi ya kile walichokiita "mpango wa uhalalishaji." Hakika, chuki ya utawala huu dhidi ya Uislamu imefikia kuwalazimisha Waislamu kuachana na mazishi ya Kiislamu na kukubali shingo upande tamaduni za Kichina za kuchoma maiti zao ambayo serikali ya Uchina inaeneza kwa kasi mkoani Xinjiang.

Pamoja na hayo, zaidi ya Waislamu wa Uyghur milioni moja wametiwa kifungoni daima katika kambi huko Xinjiang kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN), ambapo wanalazimishwa kuachana na imani yao, wanywe pombe na kula nguruwe pamoja kutoa ahadi ya utiifu kwa utawala wa kishirikina wa Chama cha Kikomunisti. Wengi wa walioko korokoroni wanateswa au kuuliwa. Fauka ya hayo, Waislamu wa Uyghur wasiopungua milioni 2 wako ndani ya "kambi za kuwafunza upya" ambapo wanalazimishwa kubeba fikra za kisiasa na kithaqafa zinazopelekea kuachana na Dini yao pamoja na kukashifu imani yao ya Kiislamu na kutamka propaganda za kikomunisti. Kwa mujibu wa AFP, moja katika nakala za serikali zinazohusiana na wale walioko katika "vitengo vya kuelimisha upya" inasema kuwa kujenga raia bora wa Uchina, vitengo hivyo lazima kwanza, "wavunje ukoo wao, wavunje mizizi yao, wavunje ushikamano wao na wavunje asili zao." Dola ya Uchina inaendesha nyumba za mayatima wa watoto wa Uyghur waliochukuliwa kutoka kwa wazazi wao ambao wako kifungoni katika kambi au wamekimbia. Katika nyumba hizi za mayatima watoto wanaelimishwa kwa njia ambayo itaondosha utambulisho wao wa Kiislamu na kuwaweka mbali na Itikadi yao ya Kiislamu. Lengo la Serikali ni kukifanya kizazi kijacho cha watoto wa Waislamu wa Uyghur kuwa watumwa watiifu walioukubali ushirikina. Tamaduni za Wachina waHan na ruwaza ya Beijing ni kuwavunja watu Waislamu wa Uyghur na kuuondosha Uislamu katika maeneo yao.

Licha ya vita hivyo vya wazi dhidi ya Uislamu vikiendeshwa na dola ya Uchina na kampeni yake ya kusafisha jamii dhidi ya watu Waislamu, kumekuwepo na kimya cha aibu kisichoshangaza kutoka kwa tawala na watawala katika ulimwengu wa Waislamu. Licha ya Serikali ya Uchina kutangaza wazi kuwa Uislamu ni "mfumo wa maradhi ya akili" na "kirusi ndani ya ubongo" haikutosha kuamsha cheche za hasira za kweli na kuitikia ndani ya watawala hawa katika serikali ndani ya ardhi za Waislamu ambao kiuwazi hawajali chochote katika matukufu ya Uislamu na maisha ya Waumini. Tawala hizi na watawala katika ardhi za Waislamu ni vifurahisho inapokuja kuwaua Waislamu ndani ya Syria, Yemen, Afghanistan, Pakistan na kwengineko… lakini wanakataa kutumia hata chembe ya kisiasa, kijeshi au kiuchumi kupatiliza kwa ajili ya Uislamu na Waislamu. Serikali ya Pakistan kwa mfano imetuma

*Endelea Uk..8*

wanajeshi 15,000 kwenda kulinda eneo la kiuchumi la ushirikiano kati ya Uchina na Pakistan na raia wa Uchina wanaofanya kazi katika miradi ya miundo mbinu katika nchi hiyo; lakini hawajaita hata mwanajeshi mmoja kwenda kulinda hadhi ya Uislamu na Ummah! Hakuna shaka Mpango wa Uchina wa Ukanda na Barabara (BRI) ambao unalenga kuwezesha biashara ya dunia ikijumuisha Asia na Mashariki ya Kati pamoja na Beijing kupitia kujenga njia za biashara ambazo zinapitia Xinjiang…zitaendeleza kununua kimya cha cha tawala hizi zilizouzwa dhidi ya serikali ya Uchina ya msalaba dhidi ya Uislamu. Huku hali halisi ikibakia, ambapo hakuna uongozi wa kikweli wa Kiislamu kusimamia matukufu ya Uislamu na Waumini. Kampeni ya kishirikina ya Uchina dhidi ya Waislamu wa Uyghur itaendelea pasi na kusimama na wataendelea kuwatesa bila wasiwasi pasi na yeyote kuwakabili. Kwa hiyo tunawauliza wale walioko katika majeshi ya Waislamu…nini ambacho kinaendelea kuwafunga kuwa na hawa watawala ambao wameuza roho zao kwa maadui wa Dini yako? Utawezaje kuishi chini ya kivuli na kutumikia uhadaifu wao? Toa nusra yako kwa dharura ili kusimamishwe Khilafah kwa njia ya Utume ambayo itanyanyua cheo chako kuwa na hadhi, shuja wa Dini yao na kuutetea Ummah wako!

إِنَّ ٱلَّذِينَ يَشۡتَرُونَ بِعَهۡدِ ٱللَّهِ وَأَيۡمَـٰنِهِمۡ ثَمَنً۬ا قَلِيلاً أُوْلَـٰٓٮِٕكَ لَا خَلَـٰقَ لَهُمۡ فِى ٱلۡأَخِرَةِ وَلَا يُكَلِّمُهُمُ ٱللَّهُ وَلَا يَنظُرُ إِلَيۡہِمۡ يَوۡمَ ٱلۡقِيَـٰمَةِ وَلَا يُزَكِّيهِمۡ وَلَهُمۡ عَذَابٌ أَلِيمٌ۬

“Hakika wanao uza ahadi ya Mwenyezi Mungu na viapo vyao thamani ndogo, hao hawatakuwa na sehemu ya kheri yoyote katika Akhera, wala Mwenyezi Mungu hatasema nao wala hatawatazama Siku ya Kiyama, wala hatawatakasa, nao watapata adhabu chungu.” [3:77]

**Imeandikwwa Kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Dr. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake**
**Katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

# Habari & Maoni
# Mateso ya Waislamu wa Uyghur: Afrika ni Mshirika Katika Uhalifu

**Habari:**

Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa (UN) zaidi wa Waislamu wa Uighur milioni moja wamekadiriwa kuwekwa kizuizini ndani ya kambi ambamo wanalazimishwa kuikashifu dini yao na kutoa ahadi ya utiifu kwa Chama tawala cha Kikomunisti cha kikafiri. Mashirika ya utetezi wa haki yameilaumu Uchina kwa muendelezo wa kampeni ya usafishaji kabila. Mnamo Agosti, shirika la habari la Washington Post lilisema kwamba ulimwengu "hauwezi kujitia hamnazo" kuhusiana na kampeni dhidi ya Waislamu. Matukufu ya Kiislamu mfano kibla katika misikiti ikibomolewa, na kwa mujibu wa shirika la habari la Associated Press, shule za dini na masomo ya Kiarabu yamepigwa marufuku na watoto kutoruhusiwa kushiriki katika shughuli za Waislamu. (https://www.aljazeera.com, 05/01/2019)

**Maoni**:

Ulimwengu wote umejumuika katika kuikashifu kisanii Uchina kutokana na sera zake za ukandamizaji wa ndugu zetu wapendwa Waislamu wa Uyghur wanaoishi Mashariki ya Turkistan. Kwa upande mwingine, Bara la Afrika limenyamaza kimya! Uongozi wa Afrika wa watawala vibaraka wamejiunga na vibaraka wenzao Waislamu kutoka katika Ulimwengu wa Waislamu ambao wamo katika hali kama yao ya kunyamaza kimya! Hakuna kiongozi ambaye amejaribu kunyanyua sauti yake au kuiotesha kidole Uchina!

Hatua ya Afrika juu ya sera za Uchina kuhusiana na Waislamu wa Uyghur inatokamana na eti ushirika wa kiuchumi kati ya bara hili na Uchina. Kufikia mwaka 2014, Uchina iliipita Amerika kwa kuwa muwekezaji Na.1 ndani ya Afrika huku takwimu rasmi zikionyesha kuwa Uchina imerekodi zaidi ya dola za marekani bilioni 250 za ushirikiano wa kibiashara na Afrika. Zaidi ya hayo, Uchina ndiyo mshirika wa kibiashara Na.1 wa nchi 138 kati ya mataifa 200 duniani. Muungano wa BRICS ulizindua Benki Mpya ya Maendeleo (NDB) iliyo na makao makuu Mjini Shanghai, Uchina na hivi majuzi 17 Agosti 2017, NDB ilifungua rasmi Kitengo cha Eneo la Afrika (ARC) mjini Johannesburg, Afrika Kusini. Benki hiyo inalenga kuifanya ARC kuwa mchangiaji mkubwa katika maendeleo ya miundo mbinu ndani ya Afrika Kusini na mshiriki muhimu katika ajenda ya maendelo ya Bara hili. Kongamano la mwisho la Ushirikiano wa Uchina na Afrika lililofanyika 3 – 4 Septemba 2018, rais wa China Xi Jinping aliahidi dola za marekani bilioni 60 kwa Bara la Afrika ikijumuisha mikopo, ruzuku na udhamini wa fedha za maendeleo. Pia Xi alitangaza mikakati minane inayolenga kuboresha mahusiano ya Uchina na Afrika ikijumuisha uwekezaji katika masuala ya afya, elimu, usalama, ubadilishanaji tamaduni na kuzidisha usafirishaji wa bidhaa zisizokuwa mali ghafi kutoka Afrika.

Ziada ni kuwa Bara la Afrika ni mjumuiko wa makoloni mengi yanayo simamiwa na watawala vibaraka watumwa waliouza roho zao kwa mabwana zao masekula wakoloni wamagharibi wakiongozwa na Marekani, Uingereza, Ufaransa na washirika wao ikijumuisha Urusi na wengineo. Wamagharibi na washirika wao hivi sasa wanapigia debe na kupitisha sheria na sera za kidhalimu za kimauaji ndani ya nchi zao zikilenga kupambana na misimamo mikali na ugaidi! Sheria na sera zao zimechukuliwa na watawala vibaraka wa Bara hili. Mfano kieneno, Makubaliano ya OAU ya Kujikinga na Kupambana na Ugaidi ya 1999, utekelezaji wa Mpango wa AU wa Kujikinga na Kupambana na Ugaidi wa 2002 na utekelezaji wa Sheria Kielekezi ya Afrika ya Kujikinga na Kupambana na Ugaidi ya 2011. Sheria Kielekezi ambayo ilibuniwa ili kuzisaidia Dola wanachama katika utekelezaji wa vipengee vilivyoko ndani ya nyenzo tofauti tofauti za kibara na kimataifa kuhusiana na kupambana na ugaidi. Hivyo basi kitaifa nchi zikapitisha sheria ikiwemo Kenya ilipitisha sheria ya Kupambana na Ugaidi ya 2012 na Mikakati ya Kitaifa ya Kupambana na Misimamo Mikali ya 2016.

Hakika yote hayo hapo juu yanadhibitisha kuwa Afrika na uongozi wake wa vibaraka watumwa hawana hadhi ya kiutu na kisiasa kuzihesabu sera za kinyama za Uchina kwa kuwa wenyewe wanajihusisha na maovu kama hayo dhidi ya raia zao Barani mote! Zaidi ya hayo, inadhibitisha kuwa Afrika haina mtizamo safi na makini wa kimfumo juu ya ulimwengu, binadamu na uhai. Kwa kuwa mfumo unaotawala ni ule batil wa kisekula wa kikoloni wa kirasilimali unaotokamana na akili finyu unaopigiwa debe na maadui wa Mwenyezi Mungu (swt) ikiongozwa na Amerika na washirika wake. Mfumo huu feki na sheria na sera zake za fujo ndio msingi wa majanga ulimwenguni kote ikiwemo majanga ya kisiasa-kijamii-kiuchumi yanayo shuhudiwa kuanzia Mashariki hadi Magharibi! Afrika imeurithi kipofupofu mfumo huu fisadi na nidhamu zake kutoka kwa mabwana zake; na hivyo hatua yake ni sawa na akili yake iliyojaa sumu na ambayo inaipa kipaombele thamani ya kiuchumi/kimada dhidi ya thamani za utu na ubinadamu!

Hatua ya dharura na msingi ambayo Afrika inatakiwa kuchukua ili kujiepusha na ushirika wa kihalifu ni kukata mahusiano na Uchina, US, UK, Ufaransa, Urusi, Ujerumani n.k ambao wote ni washirika katika kupora mali za Afrika na kuwapiga vita Waislamu na Uislamu

*Endelea Uk..10*

kwa kisingizio cha kupambana na misimamo mikali na ugaidi. Pia, wakumbatie mwito wa Khilafah ili kuikomboa Afrika kutoka katika utumwa na kusakama kisiasa-kijamii-kiuchumi hadi kupata utulivu wa kweli unaotokamana na ustawi wa kweli wa kisiasa-kijamii-kiuchumi kwa kutekeleza/kutabikisha Shari'ah (Qur'an na Sunnah) inayotoka kwa Muumba wa viumbe. Ni chini ya Khilafah pekee ambapo Afrika, Waislamu na Uislamu utapata kiukweli hifadhi ya maisha na mali zao dhidi ya wamwagaji damu duniani! Kwa kuwaunganisha wapenzi wa Jihadi ili kuwakomboa waliomo katika utumwa wa sumu ya mfumo wa kisekula wa kirasilimali. **«وَإِنَّمَا الإِمَامُ جُنَّةٌ يُقَاتَلُ مِنْ وَرَائِهِ وَيُتَّقَى بِهِ» "Hakika Kiongozi ni ngao nyuma yake mnapigana na munajilinda kupitia yeye."**

**Link ya Kampeni:**

http://www.hizb-ut-tahrir.info/en/index.php/hizbuttahrir/16793.html

**Hashtag ya Kampeni:**

#الخلافة_تحرر_تركستان_الشرقية

#Khilafah_Liberates_EastTurkestan


**Imeandikwa kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Ali Nassoro Ali**
**Mwanachama wa Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Kenya**

# Habari & Maoni
# Kizazi cha Watoto wa Uyghur Kinaibwa na Uchina

**Habari**

Utawala wa Uchina unaendelea kuwaweka watoto wa Waislamu wa Uyghur ambao wametiwa korokoroni katika kambi au walio kimbia kutokana na kuteswa na dola hiyo, katika nyumba nyingi za mayatima zinazoendeshwa na serikali ndani ya Mashariki ya Turkestan.

Kumeripotiwa watoto 500 wa Uyghur walioko kifungoni katika "shule" iliyofungwa ndani ya mji wa Kashgar pekee ambapo hawaruhusiwi kuwa na mahusiano na ulimwengu wa nje. Katika nyumba za mayatima, watoto hawa Waislamu wanapenyezewa thaqafa ya kikomunisti ili waweze kuikataa imani yao ya Kiislamu na wachukue itikadi ya ujamaa na kuwa watumwa watiifu wa dola hiyo. Tathmini ya ilani za ununuzi katika Mashariki ya Turkestan iliyofanywa na Associated Press ilipata kuwa tangu mwanzo wa mwaka 2017, serikali ya Uchina imetenga bajeti ya zaidi ya dola milioni 30 ili kujenga au kupanua takribani nyumba za mayatima 45 ili ziweze kuwa na vitanda vya kutosha kuweza kuhudumia takribani watoto 5000. Kwa mujibu wa gazeti la The Independent, mnamo Julai na Agosti mwaka jana, utawala huo ulikaribisha fursa za ujenzi wa vitengo ndani ya kaunti kadhaa mkoani humo. Ilani moja iliitisha nyumba moja katika kaunti ya Moyu iwe na ghorofa nne za mabweni ambayo yatakuwa makubwa kuliko viwanja 3 vya mpira.

**Maoni**

Utenganisho huu wa kinguvu wa watoto wa Uyghur kutoka kwa wazazi wao na familia zao ni sehemu ya msalaba wa Beijing wa kuyakata kikamilifu mafungano ya Waislamu wachanga na Dini yao na kuwabadilisha utambulisho wao- kimsingi na kimitagaa – ili kubuni kizazi chote cha Uyghur ambacho ni cha watumwa watiifu kwa Chama cha Kikomunisti na maadui wa Uislamu.

Kando na kuwafunga watoto wa Uyghur katika nyumba hizi za mayatima zinazoendeshwa na serikali, utawala wa Uchina pia umejenga maelfu ya shule za chekechea za "lugha tofauti" ili kuweza kupenyeza thaqafa kwa watoto Waislamu. 4,300 ya shule za chekechea zilijengwa au kuboreshwa ndani ya mwaka 2017 kwa mujibu wa serikali. Ndani ya taasisi hizi, watoto wanafunzwa "kuipenda Nchi yao" na kwamba dini za wazazi wao ni jambo la ajabu na lenye misimamo mikali na hivyo basi ina takiwa kuondoshwa. Imeripotiwa kuwa maafisaa mara kwa mara wamekuwa wakizuru hizi shule za chekechea na kuwauliza wanafunzi ikiwa wazazi wao wanasoma aya za Qur'an nyumbani au wanashiriki katika amali za kidini –kiukamilifu wakiwalazimisha watoto kuwachunguza wazazi wao na familia zao. Zaidi ya hayo, utawala umebuni maelfu ya shule za lugha tofauti, nyingi ambazo ni za kulala huko huko ambamo watoto wa Uyghur wanalazimishwa kuhudhuria, muda wao unadhibitiwa wasikae na wazazi wao na kuhamisha udhibiti wa malezi yao kutoka kwa familia zao za Waislamu hadi kwa serikali ya kishirikina, ambayo ina walazimisha kuishi kama wasiokuwa Waislamu wa China waHan. Gazeti la Independt liliripoti kuwa, "Ilani ya serikali iliyochapishwa Februari 2018 ndani ya mji wa Kashgar inasema kuwa watoto katika darasa la nne na kuendelea walio na wazazi walioko korokoroni lazima wapelekwe shule za bweni mara moja – hata kama mzazi mmoja yuko nyumbani. Wanafunzi lazima wamakinishwe na maadili ya kikomunisti, ilani hiyo ilisema na wafunzwe "kuipenda elimu na wawe na mapenzi ya kuifanyia kazi nchi yao" na waepuke "tabia aina 75 zinazoonyesha misimamo mikali." Serikali inasema mfano wa tabia hizo ni kama kulingania "vita vitakatifu" hadi kufuga ndevu na kuacha kuvuta sigara na kunywa pombe kwa sababu za kidini." Uyghur wengi wanahofia kuwa mbinu hizo zinasambaratisha thaqafa na utambulisho wao wa Kiislamu kutoka mtoto mmoja hadi mwengine. Inafanana na "Vizazi Vilivyoibwa" vya watoto wa Aboriginal ambao walitenganishwa na wazazi wao kinguvu na serikali mtawalia za Australia katika miaka ya 1900 na kuwekwa chini ya taasisi zinazoendeshwa na serikali ili kuondosha utambulisho wa uenyeji wao.

Kumekuwa na kelele na maandamano ya watu wa kawaida duniani kote dhidi ya Uchina kutokana na ukandamizaji wa jamii, kuwafunga mamia na upenyezaji wa thaqafa kwa Waislamu wa Uyghur wa Mashariki ya Turkestan…lakini serikali na taasisi gani zimesikia kiukweli vilio vyao na kuchukua hatua ya kusitisha uhalifu huo wa kutisha??!! Tutarajie lolote kutoka kwa mashirika kama Umoja wa Mataifa (UN) zaidi ya kawaida yake ya kutoa kauli za kukashifu ambazo hazifanyi kitu katika kumaliza janga hili? Ni zana inayofanya kazi tu kwa maslahi ya dola kubwa zilizopo katika Baraza la Usalama ambalo Uchina ni mwanachama. Urithi wake umekuwa kufeli jumla katika kuyalinda maisha ya Waislamu –ima ndani ya Syria, Ardhi Tukufu ya Palestina, Kashmir, Myanmar, Afrika ya Kati au kwengineko. Na hatutarajii lolote kutoka kwa serikali za Kimagharibi au tawala zilizoko sasa ndani ya ardhi za Waislamu ambao wanaogopa kupoteza maslahi yao ya kiuchumi na Uchina na ambao wameonyesha kwa kujirudiarudia falsafa yao ya kirasilimali –kupata maslahi ya kifedha daima yatapelekea kuondosha maangamivu na ukandamizaji wa wanadamu.

Kuna msemo maarufu wa Kiengereza unaosema kuwa, "Uwendawazimu ni kufanya jambo hilo kwa hilo na kutarajia majibu tofauti." Hakika, kama Waislamu

*Endelea Uk..12*

tunatakiwa kutambua kuwa na matumaini na UN, serikali za kibinafsi za Kimagharibi au tawala tofauti zisizokuwa za Kiislamu ndani ya ulimwengu wa Waislamu katika kuwalinda ndugu zetu wa Mashariki ya Turkestan itapelekea kufeli na kuendelea kwa maangamivu. Kuwakomboa Waislamu wa Uyghur kutoka katika makucha ya utawala wa Kichina unataka dola ambayo haipangi vitendo vyake kwa mtizamo wa maslahi ya kiuchumi bali kwa Sheria na Maamrisho ya Mwenyezi Mungu (swt) pekee, ambayo inajumuisha Agizo la (swt) la kuwalinda Waumini, pasi na kupiga hesabu za kifedha. Inataka dola ambayo kiukweli ina wakilisha na kulinda maslahi ya Uislamu na Waislamu, kuliko mashirika na serikali ambazo zinatoa shinikizo za kisanii katika kumaliza maangamivu ya wanadamu. Serikali hii ni ya Khilafah Rashidah kwa njia ya Utume ambayo Mtume (saw) ameisifu kama ngao na mlinzi wa Ummah na Dini. Tuliona kwa mfano namna chini ya uongozi wa Kiislamu, katika karne ya 8 ya Khilafah ya Ummaya, Al-Walid ibn Abd al-Malik, alipounganisha jeshi lenye nguvu la maelfu chini ya uongozi wa jenerali Muhammad ibn Qasim, kupigana na mfalme wa Hindu –Raja Dahir ndani ya Sindh, India, alipowashika mateka wanawake na watoto Waislamu. Wanajeshi Waislamu walipambana na jeshi kubwa mara kadhaa idadi yao lakini waliwashinda na kuwaokoa Waislamu wanawake na watoto kutoka kwa waliowateka na kuikomboa Sindh yote kutoka katika udikteta wa utawala wa Kihindu. Kitendo hichi hakikupigiwa hesabu za kifedha bali ni kuitikia mwito wa Mwenyezi Mungu (swt) wa kuwanusuru Waislamu kutoka katika udhalimu wazi. Kwa hiyo ikiwa twataka kumaliza madhila ya Ummah wetu ndani ya Mashariki ya Turkestan na ardhi zote duniani, basi lazima tuweke umakinifu na juhudi zetu katika udharura wa kusimamisha Khilafah Rashidah.

**Imeandikwwa Kwa Ajili ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir na**

**Dr. Nazreen Nawaz**
**Mkurugenzi wa Kitengo cha Wanawake**
**Katika Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir**

بسم الله الرحمن الرحيم

Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir Tanzania

﴿وعد الله الذين آمنوا منكم وعملوا الصالحات ليستخلفنهم في الأرض كما استخلف
الذين من قبلهم وليمكنن لهم دينهم الذي ارتضى لهم وليبدلنهم من بعد خوفهم أمنا
يعبدونني لا يشركون بي شيئا ومن كفر بعد ذلك فأولئك هم الفاسقون﴾

حزب التحرير
HIZB UT TAHRIR

REF: 04/1440 Ijumanne, 07 Jumada II 1440 H 12/02/2019 CE

# Tunaungana naa Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir Katika Kampeni Dhidi ya Ukatili wa China Kwa Waislamu Wa Turkestan Mashariki

**<u>Taarifa kwa vyombo vya habari</u>**

China ikiwa dola ya kibepari si tu inaendeleza unyonyaji kwa uroho rasilmali za nchi changa hususan za bara la Afrika na kuzitumbukiza nchi hizo katika mzigo usiohimilika wa madeni kwa ujanja wa mikopo. Bali pia China inaendeleza kampeni kali ya kiuadui na kikatili dhidi ya Uislamu na Waislamu wa Turkestan Mashariki. Eneo lililoporwa na China kwa mabavu na kulifanya kuwa sehemu yake.

Uadui wa China dhidi ya Waislamu ni athari ya chuki zake za asili katika tareekh tangu zama Utawala wa Manchu, na uadui waliotenda zama za Ukomunisti, ilhali uadui wa sasa unasukumwa zaidi na vita vya kimataifa dhidi ya Uislamu na Waislamu vinayoongozwa na madola ya Magharibi hususan Marekani. China katika zama za Ukomunisti ilishindwa kikamilifu kuifuta na kuingamiza dini ya Uislamu katika ardhi yao, licha ya kampeni yao kali na ya kikatili zama zile, hatimae Waislamu wa Uighur walipata nguvu wakaweza kuhifadhi na kulinda dini yao licha ya kuwa katika mzingiro wa hali ngumu.

Pamoja na hayo, China bado haijakata kiu yake kwa damu ya Waislamu kutoka mauwaji makubwa waliyoyatenda huko kabla, maangamizi ya taasisi za Kiislamu ikiwemo Misikiti kwa maelfu, kuuwa wanavyuoni wa Kiislamu nk. Hivi sasa inatumia mbinu tofauti tofauti kuendeleza yale yale. Inaendelea kuwaritadisha kwa nguvu Waislamu, kutenda mateso ya kimwili na kisaikologia, kuwauwa, kuwahilikisha kwa kisingizio cha ugaidi, na zaidi kuwafunga kikatili katika makambi maalumu ili kuwalazimisha waachane kabisa na kila athari ya Uislamu.

Mkakati wa China wa kuasisi makambi ya kuwafungia Waislamu ni katika mbinu ya kutaka kuondoa fungamano la Waislamu na jamii yao, na kuwatenga kando na athari za utamaduni wao (Uislamu). Hilo InshaAllah halitofanikiwa. Aidha, licha ya Ripoti ya Kamati ya Umoja wa Mataifa ya mwezi Agosti 2018 kueleza kuwa katika Jimbo la Xinjiang, kuna kambi yenye Waislamu karibu milioni kwa ajili ya kuwabadilishwa dini (BBC). Hata hivyo, kwa mujibu wa taarifa ya Muungano wa Kimataifa wa Vyuo Vikuu vya Kiislamu, idadi ya Waislamu katika makambi hayo ni kwa mamilioni. (Yenisafak)

Dhulma hii ya China kwa Waislamu wa Uighurs inatendeka ilhali hakuna hatua thabiti ya kuingilia kati kimataifa, ingawaje kuna matamshi ya kulaani hapa na pale, lakini kiuhalisia ni matamshi matupu, yakidhamiriwa kupoza tu na kuhadaa vilio vya kimataifa hususan za Waislamu, lakini kwa udhati hakuna hatua yoyote ya kivitendo.

Madola ya Magharibi yanayongozwa na Marekani, licha ya kujinadi kuwa ni vinara wa kulinda na kutetea 'haki za binadamu' lakini uzoefu unaonesha kuwa utetezi wao sio katika dhulma na majanga yanayowasibu Waislamu. Tumeshuhudia mengi katika dhulma na mateso ya Waislamu kama Afrika ya Kati, Myanmar, Kashmir, Ardhi Tukufu ya Palestine nk. Kote huko hakuna hatua zozote thabiti kukabiliana nayo.. Amma kwa upande wa nchi za Waislamu zilizotarajiwa zisimame kidete kivitendo kukinga na kukomesha uhalifu huu mkubwa, ziko kimya na nyengine zinashirikiana na wauwaji (China) kamwe ! zinajitia pambani kana kwamba haliwahusu.

*Endelea Uk..14*

Hizb ut Taahrir Tanzania inalaani uonevu na uadui  wa China kwa Waislamu wa Uighur, pia inalaani  udhaifu wa watawala wa  nchi za Waislamu katika kukabiliana na dhulma hizi. Kwa upande mwengine, tunaungana bega kwa bega na kampeni ya Afisi Kuu ya Habari ya Hizb ut Tahrir yenye kauli mbiu: "Vita vya China dhidi ya Uislamu ndani ya Turkestan Mashariki itakomeshwa na Khilafah Rashidah". Tutashirikiana katika kufedhehi matendo maovu ya serikali ya  China na pia  kufedhehi ukimya wa Biladi za Waislamu.

Tunawaombea dua zetu ndugu zetu wa kike na kiume wa jamii ya Waislamu wa Uighur wamakinishwe zaidi kwa subra katika kipindi hiki cha ukatili mkubwa.  Tunawakumbusha Waislamu wote, kuwa udhaifu wa watawala katika nchi za Waislamu ni dalili tosha ya kutofaa watawala hao kusimamia mambo na kuulinda Umma wa Kiislamu. Aidha, tunawakumbusha Waislamu wake kwa waume juu ya ufaradhi wa kufanya kazi na Hizb ut Tahrir Tanzania ili kurejesha tena dola ya Khilafah (katika nchi kubwa za Waislamu) ili kuwakomboa Waislamu wa Turkestan Mashariki na penginepo.

Tunawaomba Waislamu wote , na wote wenye hisia za ubinadamu ndani ya Tanzania na kila mahala kushiriki katika kampeni hii adhimu ili kufedhehi  ukatili  wa China kwa Waislamu wa Turkestan Mashariki.

**Masoud Msellem**
**Mwakilishi kwa Vyombo vya Habari wa Hizb ut Tahrir Tanzania**












# #الخلافة_تحرر_تركستان_الشرقية

# #Khilafah_Liberates_EastTurkestan

Email: info@uqab.or.ke




#الخلافة_تحرر_تركستان_الشرقية

#Khilafah_Liberates_EastTurkestan


Email: info@uqab.or.ke